


## 10A-Namna Ya Kuleta Isti'aadhah Na Basmalah Mwanzo Wa Suwrah:

1- **Waswlul-jamiy' - Kuziunganisha zote:** Kuzisoma kwa kuziunganisha bila kusimama baina ya Isti'aadhah, Basmalah na mwanzo wa Suwrah, kama ifutavyo:




## 2- **Waswlul-isti'aadha bil-basmalah - Kuziunganisha Isti'aadhah na Basmalah:**

Kuzisoma kwa kuziunganisha bila kusimama baina ya Isti'aadhah na Basmalah, kisha ukasimama kidogo tena ukaendelea kusoma mwanzo wa Suwrah pekee; kama ifutavyo:




3- **Qatw'ul-jamiy' - Kuzitenganisha zote:** Kuzisoma moja baada ya nyengine kuzitenganisha kwa kusimama kila baada ya moja; kama ifutavyo:



Waswlul-basmalah bis-suwrah – Kuunganisha 4- وصل البسمة بالسورة

**Basmalah na Suwrah:** Kuisoma Isti'aadhah pekee kwa kusimama kisha kuziunganisha Basmalah na mwanzo wa Suwrah kama ifutavyo:



﴿أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ﴾  
بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ﴿١﴾

### Basmalah:

Ni vyema ieleweke kuwa Basmalah ni tofauti kabisa na Isti'aadhah katika kutakiwa kusomwa kwake na msomaji wa Qur-aan. Basmalah ni *Sunnah muakkadah* (iliyosisitizwa) kwa kila anayetaka kuanza kusoma mwanzo wa Suwrah yoyote ile ya Qur-aan<sup>1</sup>, isipokuwa Suwrat At-Tawbah. Ama ikiwa anaanza kisomo chake katikati ya Suwrah yoyote ile ikiwemo Suwrat At-Tawbah<sup>2</sup> basi huwa na kхиari kuchagua apendavyo; akitaka atasoma Basmalah baada ya kumaliza kuisoma Isti'aadhah na akitaka anaweza kutosheka na Isti'aadhah.

Tamko la Basmalah ni moja tu ambayo imethibiti katika Qur-aan:

﴿إِنَّهُ مِنْ سُلَيْمَنَ وَإِنَّهُ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ﴾

((“Hakika hiyo ni kutoka kwa Sulaymaan, na hakika hiyo (imeanza na) *BismiLLahir-Rahmaanir-Rahiyim* (Kwa Jina la Allaah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu) ))<sup>3</sup>

<sup>1</sup>Ni wajibu kuileta Basmalah kila inaposomwa Suwrat Al-Faatihah kwa mtazamo wa Shaafi'iyah kwani wao wanaiona Basmalah katika Suwrat Al-Faatihah kama ni mionganini mwa Aayah zake.

<sup>2</sup>Wako baadhi ya wanazuoni waliosema kuwa haitakikani kuletwa Basmalah sehemu yoyote ile ya Suwrat At-Tawbah.

<sup>3</sup> An-Naml (27: 30)

Basmalah maana yake ni kuwa unaanza kwa Jina la Allaah Ar-Rahmaanir-Rahiym<sup>4</sup> (Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu), na kutajwa jina la Allaah katika kuanza jambo ni kupatikana baraka, kumtegemea Allaah (سبحانه وتعالى) katika kuweza kulikamilisha hilo jambo na kukubaliwa.

### Tanbih:

Basmalah inatiliwa mkazo kusomwa baada ya kumaliza kusoma Isti'aadhah ili isije kueleweka kinyume na inavyotakiwa kueleweka khasa kwa asiye na ujuzi na ufahamu wa kina wa Qur-aan, kwa sababu ataposoma Isti'aadhah kisha akasoma bila ya Basmalah mfano kauli Yake Allaah (سبحانه وتعالى) :

﴿ هُوَ الَّذِي خَلَقَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا ﴾

((Yeye Ndiye Ambaye Amekuumbieni vyote vilivyomo ardhini ...))<sup>5</sup>

Hapo italeta maana nyengine kwani dhamiri ya هو (yeye) wakati huo itakuwa inarudi kwa aliyetajwa karibu

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَنِ الرَّجِيمِ

ambaye ni *ar-rajiym* (shaytwaan aliyefukuzwa), na hii ni kinyume kabisa bali ni kupotosha maana; ndio ikawa kuileta Basmalah kama ameanza kusoma pahala kama hapa alipoisoma kwanza Isti'aadhah ni jambo litakiwalo.

---

<sup>4</sup> Ar-Rahmaan Mwingi wa Rahmah Anaowarehemu viumbe Vyake vyote, na Ar-Rahiym hii ni khasa kwa Waumini kama inavyosema Qur-aan:

﴿ وَكَانَ بِالْمُؤْمِنِينَ رَحِيمًا ﴾

((Naye kwa Waumini ni *Rahiymaa* [Mwenye Kurehemu])) [Al-Ahzaab 33: 43]

<sup>5</sup> Al-Baqarah (2: 29)